*Mulika, Na. 44 (1), 74-94*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Uchunguzi wa Dosari za Kimofosintaksia Zinazofanywa na Wajifunzaji wa Kiswahili katika Shule za Upili Nchini Uganda

*Anifah Atuhaire*[1]

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na44t1.5

**Ikisiri**

Makala haya yanawasilisha matokeo ya utafiti kuhusu dosari za kimofosintaksia zinazofanywa na wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda. Data iliyochunguzwa katika makala haya ni sehemu ya data iliyokusanywa uwandani kati ya mwezi Februari na Machi 2023 kwa ajili ya tasnifu ya uzamivu. Data hiyo ilikusanywa katika eneo la Ankole katika wilaya za Mbarara, Bushenyi na Ibanda. Sampuli ilihusisha shule sita za Mbarara, Kashaka, Igara, Nyabubare, Ibanda na Bigyera. Mbinu za uandishi wa insha, usaili pamoja na ushuhudiaji zilitumiwa kukusanya data. Watoataarifa walikuwa wajifunzaji wa Kiswahili wa kidato cha pili hadi sita pamoja na walimu wanaofundisha Kiswahili katika shule hizo. Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Usasanyuzi Dosari iliyoasisiwa na Corder, mwaka 1967. Matokeo ya uchanganuzi wa data yalibainisha kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda hufanya dosari mbalimbali za kimofosintaksia. Dosari hizo ni pamoja na matumizi yasiyo sahihi ya vipatanishi vya kisarufi, matumizi yasiyo sahihi ya viambishi, vielezi, virejeshi, vivumishi, kuchanganya njeo, utohozi usiofaa pamoja na kutokukanusha kwa usahihi. Mwandishi anatarajia kuwa, makala haya yatasaidia walimu kubaini kwamba vipengele vya kimofosintaksia kama upatanisho wa kisarufi katika njeo, urejeshaji na ukanushi, miongoni mwa vingine, huwatatiza sana wajifunzaji na kuwasababishia kufanya dosari, hivyo, ni sharti wavimakinikie sana katika ufundishaji. Hii itawasaidia wajifunzaji kuweza kuvimudu vizuri na kuwawezesha kujifunza Kiswahili kwa fasaha.

## 1.0 Utangulizi

Tafiti mbalimbali ambazo zimefanywa kuhusu ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili au lugha ya kigeni zimedhihirisha kwamba wajifunzaji hufanya dosari mbalimbali ambazo hujitokeza katika vipengele tofauti vya kiisimu. Mathalani, Mutungu (2001), Mukuthuria (2004), Rapando (2005), Hepkwony (2011), Ontiende (2013), Kisakwah (2014), Obara (2014), Ontieri (2015), Kitsao (2015), Gawasike (2016), Nyagah (2016), Vincent (2019), Vicent (2020), Kamugisha (2020), Masereka (2021) na Rutagwerela (2022), wamechunguza kuhusu dosari mbalimbali zinazojitokeza katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama L2 kwa

[1] Mwanafunzi wa Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: atuhaireanifah@gmail.com

jamiilugha tofauti. Tafiti zao zimebaini kuwa wajifunzaji hufanya dosari mbalimbali za kiisimu kama vile za kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki. Baadhi ya dosari zinazobainishwa na watafiti hawa ni pamoja na uchopekaji wa irabu, unazalishaji wa fonimu, udondoshaji wa sauti, ukiukaji wa viambishi vipatanishi vya ngeli, na matumizi yasiyo sahihi ya vivumishi, vihusishi, viunganishi, virejeshi miongoni mwa nyinginezo.

Pamoja na tafiti hizo, zipo tafiti ambazo zinaonesha kuwa kuna tofauti katika umuduji wa vipengele mbalimbali vya lugha, ambapo baadhi ya vipengele hivyo huonekana kuwa rahisi kwa wajifunzaji na vingine huonekana kuwa ni vigumu sana. Kwa vile vipengele vinavyoonekana kuwa ni rahisi, wajifunzaji hujifunza lugha kwa urahisi ilhali vile ambavyo huonekana kuwa ni vigumu, huwatatiza wajifunzaji na kuwasababishia kufanya dosari (Slabakova, 2013). Madai haya yalichochea raghba ya mtafiti kufanya utafiti wa awali kuhusu ujifunzaji wa Kiswahili kwa wajifunzaji wa shule za upili nchini Uganda ili kubaini dosari zinazofanywa na wajifunzaji na vipengele vinavyowatatiza sana katika ujifunzaji wa Kiswahili. Data za utafiti huo wa awali zilikusanywa katika shule za Bigyera na Ibanda katika eneo la Ankole lililopo Magharibi mwa Uganda kwa kuhusisha walimu wa Kiswahili na wajifunzaji wa kidato cha tatu na nne (K3 na K4) katika shule hizo. Mbinu ya uandishi wa insha, usaili pamoja na ushuhudiaji zilitumiwa kukusanya data za utafiti huo. Uchanganuzi wa data za utafiti huo wa awali uliongozwa na Nadhariatete Kikwazo iliyoasisiwa na Slabakova (2013) kwa kuegemea msingi kwamba katika ujifunzaji lugha, kuna baadhi ya vipengele ambavyo huwa ni rahisi kwa wajifunzaji na kuna vingine ambavyo huwa vigumu kujifunza. Vipengele ambavyo hujitokeza kuwa vigumu kwa wajifunzaji huwasababishia kufanya dosari kutokana na utata wa kuvimudu. Kwa hivyo, mtafiti alitumia nadhariatete hii kubainisha dosari zinazofanywa na wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda na kufafanua dosari zinazojitokeza kwa kiwango cha juu ili kubaini kipengele cha kiisimu ambacho huwatatiza sana wajifunzaji na kuwasababishia kufanya dosari katika ujifunzaji.

Matokeo ya utafiti wa awali yalidhihirisha kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda hufanya dosari katika vipengele mbalimbali ikiwa ni pamoja na kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia, kisemantiki na kimofosintaksia. Pamoja na wajifunzaji kufanya dosari mbalimbali, dosari za kimofosintaksia zilijitokeza kwa kiwango cha juu kuliko dosari za vipengele vingine. Hali hii ilidhihirisha kuwa kipengele hiki huwatatiza sana wajifunzaji katika ujifunzaji wa Kiswahili. Ni kutokana na hali hii ambapo mtafiti alipata ari ya kufanya utafiti zaidi kuhusu tathmini ya ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari nchini Uganda. Malengo ya utafiti huo yalikuwa ni kutathmini mbinu zinazotumiwa na walimu kufundishia Kiswahili, kubainisha dosari za Kimofosintaksia zinazofanywa na wajifunzaji, kueleza sababu za wajifunzaji kufanya dosari na kujadili mikakati ya kuwasaidia wajifunzaji kukabiliana na

dosari katika ujifunzaji wa Kiswahili. Hivyo, utafiti huo ndio uliozaa makala haya, yaliyolenga kubainisha dosari za kimofosintaksia zinazofanywa na wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda.

## 2.0 Methodolojia

Data za utafiti uliozaa makala haya zilikusanywa kutoka uwandani kwa kutumia mbinu ya uandishi wa insha pamoja na ushuhudiaji. Wajifunzaji walipewa zoezi la kuandika insha yenye urefu usiozidi maneno 300 juu ya kisa ambacho hawangekisahau daima. Uteuzi wa mbinu hii uliongozwa na mawazo ya Weigle (1999) Leijten na Van Waes (2013) ambao wanashauri kwamba katika kuchunguza dosari, wajifunzaji wapewe zoezi la kuandika insha yenye kiwango fulani cha maneno kinachopimika ili waweze kujieleza vizuri. Kwa kuzingatia maoni hayo, wanafunzi walipewa zoezi la kuandika insha ili ziweze kusahihishwa na kubaini dosari ambazo wangezifanya. Mbinu hii ilisaidia kupata matini zilizochambuliwa ili kubainisha dosari za kimofosintaksia zinazofanywa na wajifunzaji.

Kwa upande wa ushuhudiaji, mtafiti aliombakushiriki katika vipindi vya wajifunzaji darasani ili kujionea jinsi ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili ulivyokuwa. Kushiriki kwa mtafiti darasani kulimsaidia kushuhudia jinsi mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji darasani ulivyokuwa. Mtafiti alipokuwa akishiriki katika vipindi darasani alikuwa akirekodi masimulizi na majibu ya wajifunzaji darasani kuhusu somo. Baadaye, mtafiti alisikiliza rekodi hizo na kunukuu sehemu muhimu ambazo hatimaye zilichanganuliwa kwa lengo la kubaini dosari za kimofosintaksia zilizofanywa na wajifunzaji hao.

## 3.0 Nadharia ya Utafiti

Utafiti uliozaa makala haya uliongozwa na Nadharia ya Usasanyuzi Dosari (kuanzia sasa UD) ambayo iliasisiwa na Corder (1967). Nadharia hii inajihusisha na uchunguzi wa utendaji wa mjifunzaji kutokana na mchakato wa kiakili kutekeleza kile anachojifunza katika lugha ya pili. Kwa mujibu wa Corder (1967), usasanyuzi dosari unajihusisha na misingi mikuu mitano ambayo ni: (i) kukusanya sampuli ya kazi ya wanaojifunza lugha, (ii) kubainisha dosari, (iii) kueleza dosari, (iv) kufafanua chanzo cha dosari, na (v) kutathmini dosari. Mwandishi wa makala haya alizingatia msingi wa kwanza hadi wa tatu. Misingi hii ilimsaidia mtafiti katika kukusanya data kuhusu dosari zinazofanywa na wajifunzaji, kubainisha dosari na kueleza dosari hizo. Hii ni kwa sababu makala haya yalilenga tu kubainisha dosari za kimofosintaksia zinazofanywa na wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda. Misingi hiyo ilizingatiwa na kumwongoza mtafiti kama ifuatavyo:

i. **Kukusanya sampuli ya kazi ya wanaojifunza lugha:** Mtafiti alikusanya sampuli za kazi za wajifunzaji kutoka kidato cha pili hadi sita kwa kutumia

mbinu ya uandishi wa insha na ushuhudiaji. Kwa kutumia mbinu ya uandishi wa insha, wajifunzaji walipewa zoezi la kuandika insha kuhusu siku ambayo hawangeisahau daima. Aidha, kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji, mtafiti alihudhuria vipindi vya Kiswahili darasani na kurekodi matini simulizi kutokana na mafundisho ya darasani.

ii. **Kutambua dosari:** Insha za wajifunzaji zilisomwa na kusahihishwa ili kubainisha dosari za kimofosintaksia zilizofanywa na wajifunzaji. Aidha, data iliyorekodiwa ilisikilizwa kwa makini na kunukuliwa tungo zilizokuwa na dosari.

iii. **Kueleza dosari:** Dosari zilizobainishwa ziliainishwa kwa kuzingatia kigezo cha kimaudhui. Dosari zilizofanana kutokana na mbinu zote mbili ziliwekwa katika kundi moja na kutolewa maelezo kwa ujumla ili kujiepusha na urudiaji wa hoja kulingana na jinsi zilivyojitokeza kwenye tungo husika.

Kwa hivyo, kwa kuongozwa na Nadharia ya Usasanyuzi Dosari, matokeo ya uchambuzi wa data ni kama yalivyofafanuliwa katika sehemu inayofuata.


## 4.0 Dosari za Kimofosintaksia Zinazofanywa na Wajifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Pili katika Shule za Upili Nchini Uganda

Kutokana na data za utafiti zilizokusanywa kwa kutumia mbinu ya uandishi wa insha na ushuhudiaji, ilibainika kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda hufanya dosari mbalimbali katika ujifunzaji wao. Makala haya yamelenga kubainisha na kueleza dosari za kimofosintaksia zinazofanywa na wajifunzaji hao. Matokeo ya uchambuzi wa data yamedhihirisha kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda hufanya dosari mbalimbali za kimofositaksia. Zifuatazo ni baadhi ya dosari hizo:

### 4.1 Matumizi Yasiyo Sahihi ya Vipatanishi vya Kisarufi vya Nomino

Kutokana na uchambuzi wa data zilizokusanywa kutoka kwa wajifunzaji kwa kutumia uandishi wa insha na ushuhudiaji, ilibainika kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda hufanya dosari kutokana na matumizi yasiyo sahihi ya vipatanishi vya nomino mbalimbali. Mifano ya tungo zilizobainika kuwa na dosari za aina hii ni kama ilivyo katika insha ifuatayo:

**Insha Na. 1**



6. Tunga insha yenye maneno yasiyozidi 300 juu ya siku ambayo hutaisahau daima.

SIKU ZA MAZALIWA YANGU

Siku mimi sitasahau daima ni siku ya ~~#~~ sherehekea mazaliwa yangu.

Siku moja asubuhi siku ya P.5 shule ni niko domu nalala. Nilisikia kangazo chaita jina langu "Arinda your parent is here come please" Hiyo siku nilipata furahi mingi. Mama enapeleka nyumba nikaona mipango inaendelea hapa na hapa. God! Ninashangaa nikafuliza kuna nini? Niliona watu wingi nyumbani yote enafurahi nyingi sana. Nkasema kuna nini kwa mutima yangu. Wantu wengine wanaendelea wanakuja. Watu yote enatuka nini hapa? Sherehe ya nini?

Dada wangu Sarah alikuja akamwagia maji mimi na kutema happy Birthday Arinda!'! Hoo! ni siku ya mazaliwa. mimi ~~siku~~ sijui hata. Nicheka sana dada ekaleta chakula nyumbani. Nilikukula sana na chakula elikuwa tamu sana.

Mama yangu mingine jina lake enaitwa Zahara anakuja na gari yake ya ALFAD ~~b~~ hiyo gari kubwa enabeba wantu wingi. Tulienda na kukaa gari. Gari elienda kwa speed sana tukafika kwebukona kwa muda nchache. Tuliona watu wingi mbarara mjini na mama Zahara ekapeleka mimi dukani kubwa ekasema chagua kitu ~~yote~~ yote onataka. Nilichagua nyata nzuri ya black yenye ncoaso.

Baadani, alipeleka sisi hoteli kubwa ina swimming pool ili kuwanau hapo. Tulifurahi mzuri sana na kurudia nyumba. Usiku sawa sita.

Asante sana.

Jina yangu ni Arinda Kakibu.

S.6A.

**Chanzo:** Data kutoka Uwandani (2023)

Data hii inadhihihirisha dosari mbalimbali zilizofanywa na mjifunzaji kutokana na matumizi yasiyo sahihi ya vipatanishi vya nomino alizozitumia katika insha hii. Aidha, kutokana na data zilizokusanywa kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji, dosari za aina hii pia zilijitokeza. Kwa mfano, katika masimulizi yafuatayo mjifunzaji akisimulia kuhusu siku ambayo hangeisahau daima, anasema:

**Simulizi Na. 1**

…siku nvua *elinyesha sana na gari nyingi *zilikuwa *zinaterera sana kwa muda. Tulienda polepole lakini mbele tulipata ajali mbaya. Gari *imegonga ngombe kwa sababu ngombe *ilikuwa katikati barabarani. Sehemu iyo *elikuwa na ngombe *nyingi *zikitoka huku na huku …

**Chanzo:** Data kutoka Uwandani (2023)

Katika data hii, sehemu ambazo zimewekewa alama (*) zinabainisha dosari zilizotokana na matumizi ya vipatanishi vya kisarufi visivyo sahihi kwa nomino zinazorejelewa.

Kutokana na data hizi, dosari za kimofosintaksia zinazobainika zimeoneshwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali Na. 1: Dosari Kutokana na Matumizi Yasiyo Sahihi ya Vipatanishi vya Kisarufi**

| Na. | Tungo zenye Dosari | Tungo katika Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|
| a) | Nilisikia tangazo **enaita* | Nilisikia tangazo linaita |
| b) | Mipango **jinaendelea* | Mipango inaendelea |
| c) | Niliona *wantu *wingi* | Niliona watu wengi |
| d) | *Wantu *wingine* | Watu wengine |
| e) | Chakula **elikuwa* | Chakula kilikuwa |
| f) | Jina lake **enaitwa* | Jina lake anaitwa |
| g) | Gari **elienda* | Gari lilienda |
| h) | *Viyato *nzuri* | Viatu vizuri |
| i) | *Mvua *elinyesha* sana | Mvua ilinyesha sana |
| j) | *Gari *nyingi zilikuwa* | Magari mengi yalikuwa |
| k) | *Ngombe *ilikuwa* katikati | Ng’ombe alikuwa katikati |
| l) | Sehemu **iyo elikuwa* | Sehemu hiyo ilikuwa |
| m) | *Ngombe *nyingi zikitoka* | Ng’ombe wengi wakitoka |

**Chanzo:** Data kutoka Uwandani (2023)

Kutokana na mifano iliyomo katika Jedwali Na. 1 hapo juu, wajifunzaji walifanya dosari kwa kutumia vipatanishi visivyo sahihi katika nomino tofauti. Hebu tuangalie mifano ifuatayo:

Katika tungo (a), kipatanishi “e” kilitumiwa kurejelea nomino *tangazo* badala ya “li”. Katika (b) badala ya mjifunzaji kutumia kipatanishi “i” kwa nomino *mipango,* alitumia “ji” ambacho si sahihi. Katika tungo (c) na (d), nomino *watu* ilirejelewa kwa kutumia kipatanishi “wi” badala ya “wa”. Vilevile, katika (e), nomino *chakula* ilirejelewa kwa kutumia kipatanishi “e” badala “ki”.

Halikadhalika, katika (g) na (j), nomino *gari* imerejelewa kwa kutumia vipatanishi “i” na “zi” ambavyo si shihi badala ya “li” na “ya” kwa umoja na wingi. Pia,


katika “h”, nomino *viatu* imerejelewa kwa kutumia “n” badala ya “vi” na kusema “*viyato nzuri*” badala *ya “viatu vizuri”.* Katika tungo (l) mjifunzaji alitumia “e” badala ya kipatanishi “i” kwa nomino *sehemu* na badala ya tungo kuwa “*sehemu iyo elikuwa*” angesema “*sehemu hiyo ilikuwa”*

Aidha, katika (k) na (m), nomino *ng’ombe* ingerejelewa kwa kutumia kipatinishi “a” kwa umoja na “wa” kwa wingi. Mjifunzaji badala ya kutumia vipatanishi hivi, alitumia “i-zi” ambavyo si vipatanishi sahihi vya nomino zinazotaja viumbe vyenye uhai. Kwa hivyo, kutokana na maelezo haya, ni dhahiri kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda hufanya dosari za kimofosintaksia kutokana na matumizi ya vipatanishi visivyo sahihi.

**4.2 Dosari Kutokana na Matumizi ya Viambishi vya Nomino Vasivyo Sahihi**

Kutokana na data za uwandani zilizokusanywa kwa kutumia uandishi wa insha, ilibainika kuwa wajifunzaji pia hufanya dosari kutokana na matumizi yasiyo sahihi ya viambishi vya nomino vya idadi ya umoja na wingi. Kwa mfano, katika insha ifuatayo, dosari za aina hii zinajitokeza kama ifuatavyo:

**Insha Na. 2**


SIKU AMBAYO HUTASAHAU DAIMA


Natoka kwa shuleni na kuenda kutika nyumbani kutafuta school fees. nyumba ilikuwa imefungwa.
Nano kuwa bila kifunguo mama yeye anaenda na kifunguo kyake wakati yote nkufili infunya mulango na sina kya kufanya sasa.
Nauliza naiba anaambia mama ameenda kwa chikundi yao ya wanawake ya pesa
Naiba alisoma mimi njoo katika nyumbani wake. Naingia
Nakasikia chitu kyikwani inasema ingia, hapana.
Mimi naogopa wantu ya kijiji kyetu ana itina mingi sana hata analoga wantu. Nasama nifanye nini?,
Sasa nina, enangesha mingi ina maiiwe mingi. Hapana kya kufanya nkaingia munyumbani?
Ninatetema sana miguu jangu ananipa kyakula nasema hafema njaa.

**Chanzo:** Data kutoka Uwandani ( 2023)

Data hii, inadhihirisha dosari za kimofosintaksia zilizotokana na wajifunzaji kwa kutumia viambishi vya nomino visivyo sahihi. Hata anwani ya insha hii mwandishi ameshindwa kuihusisha na nafsi ya kwanza umoja badala yake

ametumia nafsi ya pili umoja. Ufuatao ni mfano mwingine wa insha yenye dosari za aina hii:

**Insha Na. 3**


Siku ambayo sitashau Daima
Ililaiwa sika kuu ya chrismas na tulifural sana kuselebratinga mazalibuaa ya yesu kuristo.
Hiyo siku ndfuraha sana. tuli kulifumba kila chitu chizuri kya kura na kunya.
Chakula chilikwoa chizuri lakini chakutosha.
Bagenyi bote balikuja iyo siku na kufurahi
Anko wangu wa kyama kya polisi alikuja na famile yake vweli kueli sisi yote ilifurai sana.

**Chanzo:** Data kutoka Uwandani (2023)

Data hii inabainisha kuwa matumizi ya viambishi awali vya nomino visivyo sahihi viliathiri maneno mengine katika tungo nzima na kusababisha dosari za kimofosintaksia. Kwa ujumla, kutokana na data hizi, dosari zinazojitokeza zimeoneshwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali Na. 2: Dosari Kutokana na Matumizi ya Viambishi vya Nomino Visivyo Sahihi**

| Na. | Tungo zenye Dosari | Tungo katika Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|
| a) | **Kifunguo kyake* | Ufunguo wake |
| b) | **Nkufuli ifunga* mlango | Kufuli limefunga mlango |
| c) | **Bagenyi bote* | Wageni wote |
| d) | **Kyama kya* polisi | Chama cha polisi |

**Chanzo:** Data kutoka Uwandani (2023)

Tungo zilizomo katika Jedwali Na. 2 kama zinavyobainika katika Insha Na. 2 na 3), zinadhihirisha kuwa wajifunzaji walitumia viambishi vya nomino visivyokuwa sahihi na kuathiri matumizi ya viambajengo vingine katika tungo nzima. Kwa mfano, katika (a), mjifunzaji alitumia kiambishi awali *"ki*" badala ya *"u"* kwa nomino *"-funguo"*. Matumizi ya kiambishi *"ki"* yaliathiri kimilikishi kilichotumiwa na badala ya kuwa *"wake"* kikiwa *"kyake"*. Vilevile, *katika* (b)*,* kiambishi *"n"* kwa mzizi wa neno *"kufuli"* kilitumiwa na kuathiri kitenzi *"funga"* kilichotumiw*a,* yaani *"ifunga"* badala kutumia *"limefungwa"*. Katika mfano (c), kiambishi 'ba" kisicho sahihi kilitumika kwa mzizi wa nomino "-geni" badala ya "wa". Hili pia liliathiri kiidadi kilichotumiwa katika tungo hiyo, badala ya kuwa "wote" mjifunzaji alisema "bote".

Kwa hivyo, kulingana na mifano hii ya tungo, ni dhahiri kuwa wajifunzaji hufanya baadhi ya dosari za kimofosintaksia katika ujifunzaji wao wa Kiswahili kutokana na matumizi yasiyo sahihi ya viambishi vya nomino husika.

**4.3 Dosari Kutokana na Matumizi Yasiyo Sahihi ya Vielezi vya Mahali**

Wajifunzaji pia walifanya dosari zilizotokana na kutumia vielezi visivyokuwa sahihi katika tungo zao. Kutokana na data zilizokusanywa kupitia uandishi wa insha na ushuhudiaji, ilibainika kuwa wajifunzaji hufanya dosari kwa kushindwa kutumia vielezi sahihi. Mifano ya tungo zenye dosari za aina hii inajitokeza katika nukuu ifuatayo kutokana na masimulizi ya mjifunzaji wa kidato cha tano. Anasema:

**Simulizi Na. 2**

> …nilianzia *katika shuleni kidatoni moja kujifunza lugha ya swahili . Nilipofika katika shuleni niliona wanafunzi wingi *katika shuleni. Nilifika *kudarasa na wanafunzi alikuwa wingi sana. Niligopa *kuingiamu nkataka kwenda *katika nyumbani. Hapo niliona kanisa *mushule nikataka kwenda *kukanisa nijifiche

**Chanzo:** Data kutoka Uwandani (2023)

Data hii ina tungo ambazo si sahihi kimofositaksia kutokana na matumizi yasiyo sahihi ya vielezi vya mahali. Mifano ya tungo hizo imeoneshwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali Na. 3: Matumizi ya Vielezi vya Mahali Visivyo Sahihi**

| Na. | Tungo zenye Dosari | Tungo katika Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|
| a) | Nilianzia **katika shuleni kidatoni* | Nilianzia shuleni katika kidato |
| b) | Nilifika **kudarasa* | Nilifika darasani |
| c) | *Niligopa *kuingiamu* | Niliogopa kuingia ndani |
| d) | Niliingia **kwa darasani* | Niliingia darasani |
| e) | Niliona kanisa **mushule* | Niliona kanisa shuleni |

**Chanzo:** Data kutoka Uwandani (2023)

Tungo zilizomo katika Jedwali Na. 3 hapo juu zina dosari za kimofosintakisia kutokana na matumizi tofauti ya vielezi ambavyo si sahihi. Dosari hizi zimefafanuliwa zaidi katika vipengele 4.3.1 na 4.3.2 vifuatavyo:

#### 4.3.1 Matumizi ya Kielezi [kwa], [katika] pamoja na [ni] katika Kurejelea Mahali

Kutokana na mifano iliyooneshwa katika Jedwali Na. 3 kama ilivyonukuliwa kutokana na masimulizi ya mjifunzaji, kunadhihirika matumizi yasiyo sahihi ya vielezi vya mahali. Kwa mfano, katika (a), mjifunzaji anatumia kielezi [katika] pamoja na mofu [ni], yaani "*katika shuleni*" badala ya kusema "*shuleni*". Pia, katika mfano (d), kuna matumizi ya kielezi [kwa] na [ni] kwa pamoja kuelezea mahali *"darasani"*. Katika Kiswahili *"kwa"* au *"katika"* ni vielezi na haviwezi kujitokeza katika tungo moja pamoja na *"ni"* ambayo pia ni mofu inayojitokeza kama kiambishi tamati kwa mzizi wa nomino na kuifanya nomino hiyo kubadilika na kuwa kielezi cha mahali. Kwa hivyo, kutokana na data hizi, matumizi ya [kwa/katika] pamoja na [ni] katika tungo yalisababisha tungo hizo kutokuwa sahihi kimofosintaksia.

#### 4.3.2 Matumizi ya "mu"/"ku" kama Kielezi cha Mahali

Mbali na matumizi ya [kwa/katika] pamoja na [ni] katika tungo moja, wajifunzaji pia walifanya dosari kwa kutumia mofu [mu] na [ku] kama vielezi vya mahali. Kwa mfano, katika (c), mjifunzaji alifanya dosari aliposema " *...niligopa kuingiamu...*". Katika tungo hii, mjifunzaji alitumia "mu" kama kiambishi tamati kwa kitenzi *"-ingia"* kwa maana ya *"kuingia ndani*".

Kadhalika, katika mfano (e), kuna matumizi ya kiambishi awali "*mu"* mbacho pia kilitumiwa kama kielezi cha mahali. Mjifunzaji alisema *"...niliona kanisa mushule..."* badala ya kusema *"...niliona kanisa shuleni..."*. Hivyo, kutokana na mifano hii, ni dhahiri kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda hufanya dosari za kimofosintaksia kutokana na matumizi ya vielezi vya mahali ambavyo si sahihi.

### 4.4 Dosari Zinazotokana na Matumizi Yasiyo Sahihi ya Virejeshi

Data zilizokusanywa kutoka uwandani pia zilidhihirisha kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda hufanya dosari kutokana na kushindwa kutumia virejeshi sahihi. Kwa mfano, katika masimulizi ya mjifunzaji wa kidato cha tano kuhusu riwaya ya *Kufa Kuzikana* katika somo la fasihi, alitoa majibu yenye tungo zenye virejeshi vya nomino mbalimbali visivyokuwa sahihi. Mifano ya tungo hizo inaoneshwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali Na. 4: Matumizi Yasiyo Sahihi ya Virejeshi**

| Na. | Tungo zenye Dosari | Tungo katika Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|
| a) | Riwaya **iliyeandikwa* | Riwaya iliyoandikwa |
| b) | Riwaya **ambaye* | Riwaya ambayo |
| c) | **Waliyokuwa* na | Waliokuwa na |
| d) | Urafiki **uliyokuwa* | Urafiki ambao |
| e) | Matatizo **ambazo* | Matatizo ambayo |

**Chanzo:** Data kutoka Uwandani (2023)


Kutokana na data hizi, mjifunzaji alifanya dosari kwa kutumia virejeshi visivyokuwa sahihi kurejelea nomino za ngeli tofauti. Kwa mfano, katika (a) na (b), kirejeshi "ye" kinatumiwa kurejelea nomino *riwaya* badala ya "yo". Kisarufi "ye" ni kirejeshi kinachotumiwa kurejelea viumbe vyenye uhai katika hali ya umoja, na kwa hiyo kukitumia kurejelea nomino *riwaya* si sahihi. Isitoshe, katika (c), kirejishi "yo" kimetumika kurejelea *watu* badala ya kutumia "o", katika mfano (d), nomino *urafiki* inarejelewa kwa kutumia "yo", yaani " *urafiki uliyokuwa*" badala ya *"urafiki uliokuwa"*. Vilevile, katika (e), kirejeshi "zo" kinatumiwa kurejea nomino *matatizo* kwa kusema *"matatizo ambazo"* badala ya kutumia "yo" na kusema *"matatizo ambayo"*.

Kwa hivyo, kutokana na mifano hii, ni dhahiri kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini uganda hufanya dosari za kimofosintaksia kutokana na kushindwa kutambua kirejeshi sahihi cha nomino husika katika tungo. Virejeshi vinavyotumiwa katika tugo hizi ni vya Kiswahili ingawa havijatumiwa kwa usahihi kurejelea nomino zinazohusika katika tungo.

### 4.5 Matumizi Yasiyo Sahihi ya Njeo

Data zilizokusanywa kwa kutumia uandishi wa insha zinadhihirisha kuwa wajifunzaji hufanya dosari kutokana na matumizi yasiyo sahihi ya njeo. Wajifunzaji walichanganya njeo kimatumizi ambapo tungo zao zilidhihirisha matumizi ya njeo /ta/, /me/ na /na/ badala ya /li/ ya wakati uliopita, "lime" badala ya "li" na nyinginezo. Mifano ya tungo zenye dosari zinazotokana na matumizi yasiyo sahihi ya njeo kama zilivyobainika katika kazi za wajifunzaji. Hebu tuangalie katika insha ifuatayo:

**Insha Na. 4**


6. Tunga insha yenye maneno yasiyozidi 300 juu ya siku ambayo hutaisahau daima.

SIKU AMBAYO SINASAHAU DAIMA
Siku ambayo sinasahau
Daima mimi naenda na jomba mjini.
Mimi na Jomba tunakuenda kampala mimi siku moja
kwenda fasi hiyo Huko minafurahi mingi sana tunaona
wantu wingi motoka nyingi, na nyumba nakuwa ndefu.
Nauliza jomba kwamba haya manyumba ndefu wanapanda
Vipi? Ānacheka na jomba anasemaa wacha weewe!
Mambo za Kampala unauliza kintu yote yote. Unaliza
ukifika kwa nyumbani. Hiyo siku mimi kwali siñasahau
maisha yangu kwa ku fanya mime ninafurahi sana
Nimimi anaitwa
ARIALIA NANKUNDA

**Chanzo:** Data kutoka Uwandani (2023)

Data hii inadhihirisha kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda hufanya dosari za kimofosintaksia kutokana na matumizi yasiyo sahihi ya njeo. Mifano ya tungo zenye dosari za aina hii imebaininishwa kwenye Jedwali Na. 5 lifuatalo:

**Jedwali Na. 5: Dosari Kutokana na Kuchanganya Njeo**

| Na. | Tungo zenye Dosari | Tungo katika Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|
| a) | Siku ambayo **sinasahau* | Siku ambayo sitaisahau |
| b) | *Mimi na jomba *tunaenda* mjini | Mimi na mjomba tulipoenda mjini |
| c) | **Tunaona wantu wingi* | Tuliona watu wengi |
| d) | **Ninauliza jomba* | Nilimuuliza mjomba |
| e) | *Jomba *anasema* | Mjomba alisema |

**Chanzo:** Data kutoka Uwandani ( 2023)

Katika tungo (a), mjifunzaji alitumia njeo “na” badala ya “ta”, na kusema “sinasahau” badala ta “sitaisahau”. Katika (b) mjifunzaji alitumia njeo ya wakati uliopo badala ya wakati uliopita , na kusema “tunaenda” badala ya “tulienda”. Katika (c) njeo iliyopo pia ilitumiwa badala ya iliyopita, yaani “tunaona” badala ya “tuliona”. Kutokana na tungo (d), mjifunzaji alitumia njeo iliyopo badala ya iliyopita kwa kusema “ninauliza” badala ya “nilimuuliza”. Kwa hivyo, ni dhahiri kuwa mjifunzaji katika insha yake alichanganya njeo hizi na kuifanya isomeke katika wakati uliopo badala ya wakati uliopita.

Kadhalika, dosari kutokana na matumizi yasiyo sahihi ya njeo pia zilibainika katika data zilizokusanywa kwa kutumia ushuhudiaji ambapo mjifunzaji alinukuliwa katika majibu yake akisema:

**Simulizi Na. 3**

> …Akida *alimekuwa rafiki wake wa zamani na dhati na Tim. Hiki kinaonekana alipokuwa Mkanju na Tim Mkorosho na Wakorosho *watasumbua wakanju, hata baba wake Tim *alimeua baba wa Akida lakini Akida *alimesamehe yeyee Tim rafiki…
>
> **Chanzo:** Data kutoka Uwandani (2023)

Katika data hii, mjifunzaji alifanya dosari kwa kuchanganya njeo, pale alipotumia "lime", ta" na "na" badala ya njeo iliyopita "li".

Kutokana na data hizi, ni bayana kuwa wajifunzaji wanazitambua mofu mbalimbali zinazotumiwa katika lugha ya Kiswahili kurejelea vipindi tofauti vya wakati, ila, bado hawana ujuzi wa kuzitumia kutunga sentensi sahihi. Data hizi zinabainisha kuwa wajifunzaji wanashindwa kutambua njeo ipi itumiwe kurejelea wakati maalumu, na kwa hivyo, huzichanganya kimatumizi.


### 4.6 Matumizi Yasiyo Sahihi ya Vivumishi

Matokeo ya uchambuzi wa data za utafiti zilizokusanywa kwa kutumia uandishi wa insha pamoja na ushuhudiaji yalionesha kuwa, miongoni mwa dosari zilizofanywa na wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda pia, kuna zile zinazotokana na matumizi yasiyo sahihi ya vivumishi. Dosari hizo zinaelezwa katika vipengele vifuatavyo:

#### 4.6.1 Matumizi Jumuishi ya Vivumishi Viulizi

Data zilizokusanywa zinabainisha kuwa wajifunzaji hufanya dosari kwa kutumia viulizi kiholela bila kuzingatia nomino inayorejelewa. Kwa mfano, kutokana na data zilizokusanywa kwa kutumia uandishi wa insha pamoja na ushuhudiaji, ilibainika kuwa wajifunzaji walifanya dosari kutokana na kushindwa kutumia viulizi mwafaka. Mifano ya tungo zenye dosari za aina hii imebainishwa katika data zifuatazo:

**Insha Na. 5**


6. Tunga insha yenye maneno yasiyozidi 300 juu ya siku ambayo hutaisahau daima.

Siku AMBOYO SIIASAHAU

Mimi naitwa Kananura Alais Kareen Nianenda kusema hadithi ya siku sitasahau. Niliienda na rafiki wangue swaliki kucheza "football match" na kutoloka shuleni.

Jamani siku iyo inakuwa na tabu sana, tunakuindi domu kulala na askari na Hedimasta yako hapo domitory.

Kujakuja hapa Head master akapiga kelele. Tuliopa tatuna kitu nini ya kufanya. Askari anakamata sisi. Onalimbia fasi nini unatoka. Sema jina yako ni nini? sema tumbavu wewe. wenzako wingine amekimbia fasi gani? Wewe mtoto wa mzee gani unakuja fanya fujo? Wewe baba wako anaitwa nini?"

Huyo askari alikuwa askali au sitani mimi sijui hiyo siku jamani napata matatizo.

Ninanyamanza natubin HM anasema nini? anasema mimi leta mzazi yako? anasema kitu gani au nini mimi tafanya.

**Chanzo:** Data kutoka Uwandani (2023)

Katika data hii kuna dosazi za matumizi ya viulizi visivyo sahihi. Dosari kutokana na matumizi yasiyo sahihi ya viulizi pia zilibainika katika data zilizokusanywa kwa kutumia ushuhudiaji. Kwa mfano, mjifunzaji wa kidato cha nne alipokuwa akisimulia kisa kuhusu siku ambayo hangeisahau daima, alitumia kiulizi “nini?” kuuliza maswali yote yaliyohusika. Alisema:

**Simulizi Na. 4**

> ...mtoto onakuja kushule na mavili kama hii kwa nini? Na tena onachelewa. Nkasema samahani natoka mbalimbali sana. Sasa mwalimu mkuu nauliza tena, jina yako ni nini? Nikasema ni Ivan Sunday. Unatoka nini? Ninasema Ishaka, Kwenu ni nini? Baba wako unaitwa nini?...

**Chanzo:** Data kutoka Uwandani (2023)

Data hizi kwa ujumla zinadhihirisha kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda hufanya dosari kutokana na matumizi yasiyo sahihi ya vivumishi viulizi. Dosari zinazojitokeza katika data hizi zimeoneshwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali Na. 6: Matumizi Jumuishi ya Vivumishi Viulizi**

| Na. | Tungo zenye Dosari | Tungo katika Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|
| a) | **Kintu nini ya kufanya?* | Kitu gani cha kufanya |
| b) | **Fasi nini unatoka?* | Unatoka wapi? |
| c) | **Jina yako ni nini?* | Jina lako ni nani? |
| d) | *wingine *amekimbia fasi gani?* | Wengine wamekimbilia wapi? |
| e) | **Kwenu ni nini?* | Kwenu ni wapi? |
| f) | *Baba wako *anaita nini?* | Baba yako anaitwa nani? |


**Chanzo:** Data kutoka Uwandani (2023)

Kutokana na tungo zinazobainishwa katika jedwali hili, mjifunzaji alitumia kiulizi *"nini"* bila kujali kile kinachoulizwa. Badala ya kutumia "*nini"* pekee, angetumia viulizi vingine kulingana na nomino husika. Kwa mfano, katika (a) mjifunzaji angetumia kivumishi kiulizi *gani?* Badala ya *nini,* katika (b) na (d), kinachoulizwa ni mahali na kwa hivyo, kiulizi *wapi* kingefaa badala ya *nini.* Vilevile, katika (c) na (f) *mjifunzaji angetumia nani* na kutunga tungo kama "*jina lako ni nani?"* na "*Baba yako anaitwa nani".* Aidha, katika tungo (e), mjifinzaji angetumia kiulizi wapi badala ya lini na kusema "*kwenu ni wapi*" badala ya kusema "*kwenu ni nini*". Kwa hivyo, kutokana na tungo hizi, ilibainika wazi kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda hufanya dosari kutokana na matumizi yasiyo sahihi na vivumishi viulizi.

### 4.6.2 Matumizi Yasiyo Sahihi ya Vivumishi Vioneshi

Wajifunzaji pia hufanya dosari kutokana na kutokutumia vivumishi vioneshi vilivyo sahihi kulingana na nomino inayorejelewa. Hii inabainika katika data za utafiti zilizokusanywa kwa kutumia uandishi wa insha, ambazo zilidhihirisha kutatizika kwa wajifunzaji kuhusu matumizi ya vioneshi. Mifano ya dosari za aina hii inabainika katika insha ifuatayo:

**Insha Na. 6**



6. Tunga insha yenye maneno yasiyozidi 300 juu ya siku ambayo hutaisahau daima.

Jina langu ni Makama Jean nakuandika insha huu kuhusu ambayo hutuisahau daima. Siku huu ni siku mimi nataenda kufanya maswali wangu wa Primare siku hiyo.

Wakati iyo mimi ninaguya wa jana baba anapeleka kwa datari

Daktari huo anapatia dawa mimi

Mimi nakwenda katika gari ya taksi kwa shuleni ya Ibanda junior fasi apoapo wanafunzu wa United parents kwenda kufundisha maswali huu Muda hii fasi hiyo ina wafunzi wingi na ili kitu ya kufanya maswali, wanafunza wa shuleni huenda katika taksi ya Ibanda junior School. Nguwa anayasha kabisa na mipango hayo ya maswali ya UNEB inasonga mbele.

Hilo siku nilifanya maswali wa katarasi huu kuwa raisi na maswali mengi 50% juu ya 100%

Wanafunzi hayo nyingi walia karatasi ya Sayansi ina Maswali magumu

Nanaomba Mungu nihapita maswali hayo.

Asante bibi
Chris

**Chanzo**: Data kutoka Uwandani (2023)

Kutokana na data hii, inadhihirika kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda hufanya dosari mbalimbali za kimofosintaksia kutokana na matumizi yasiyo sahihi ya vivumishi vioneshi. Mifano ya tungo zenye dosari za aina hii imeoneshwa katika Jedwali Na. 7 lifuatalo:

**Jedwali Na. 7: Vionyeshi Visivyo Sahihi**

| Na. | Tungo zenye Dosari | Tungo katika Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|
| a) | Wakati **iyo* | Wakati huo |
| b) | Daktari **huo* | Daktari huyo |
| c) | *Muda *hii* | Muda /wakati huu |
| d) | *Fasi *hilo* | Sehemu ile/nafasi ile |
| e) | **ile kintu* | Kitu kile |
| f) | *fasi *apoapo* | Mahali papohapo |
| g) | Mipango **hayo* | Mipango hiyo |
| h) | **Hilo siku* | Siku hiyo |

**Chanzo:** Data kutoka Uwandani (2023)

Kulingana na taarifa hii, wajifunzaji walifanya dosari kwa kutumia vionyeshi visivyo sahihi kurejelea nomino na hali tofauti, kwa mfano, katika (a) kionyeshi *"hiyo"* kilichotumiwa kuashiria wakati si sahihi na badala yake *"huo"* kingetumiwa. Kadhalika, katika (b) nomino *daktari* ingeashiriwa kimuktadha wa matumizi kwa kutumia kioneshi "huyo" badala ya "huo", katika (c) nomino muda ingeashiriwa kwa kutumia "huu" badala ya "hii". Vilevile, katika (e) kioneshi

"kile" kingetumiwa badala ya "ile" kuashiria "ki", katika (g) kioneshi sahihi ambacho kingetumiwa ni "hiyo" badala ya "hayo" na katika (h) nomino siku ingerejelewa kwa kutumia kioneshi *"hiyo"* badala ya "*hilo"*.

Kutokana na tungo hizi, imebainika kuwa wajifunzaji hushindwa kutumia vivumishi vioneshi vya nomino vilivyo sahihi na kufanya dosari za kimofosintaksia kwa kutotumia kirejeshi sahihi kurejelea nomino husika katika tungo zao.

**4.6.4 Dosari Kutokana na Matumizi ya Kivumishi Kisifa**

Katika matumizi ya vivumishi visifa, wajifunzaji walifanya dosari kwa kushindwa kutumia kiambishi sahihi cha nomino kwa mzizi wa kivumishi. Baadhi ya dosari za aina hii zilizobainika kutokana na insha pamoja na masimulizi yaliyorekodiwa kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji ni kama zifuatazo:

**Jedwali Na. 8: Kivumishi Kisifa Kisicho Sahihi**

| Na. | Tungo zenye Dosari | Tungo katika Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|
| a) | Kitu* *nzuri* | Kitu kizuri |
| b) | Kaz*i *mzuri* | Kazi nzuri |
| c) | Nguo **jeusi* | Nguo nyeusi |
| d) | Nyumba **warefu* | Nyumba ndefu/majengo marefu |
| e) | Barabara **zuri* | Barabara nzuri |
| f) | Chakula **nzuri* | Chakula kizuri |
| g) | Pahali **nkubwa* | Pahali pakubwa |
| h) | Rinda **ndefu* | Rinda refu |
| i) | Viatu **nzuri* | Viatu vizuri |
| j) | *Swahili *mzuri* | Kiswahili kizuri |

**Chanzo:** Data kutoka Uwandani (2023)

Data hii inabainisha wazi kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda hufanya dosari kutokana na matumizi yasiyo sahihi ya vivumishi visifa. Kwa ujumla, dosari zinazooneshwa katika jedwali hili, zinajitokeza wakati wajifunzaji wanaposhindwa kutambua viambishi sahihi vya nomino zinazovumishwa, na kutumia vibishi visivyo sahihi kwa mzizi wa kivumishi kisifa.

**4.7 Dosari Kutokana na Mpangilio Usio Sahihi wa Viambajengo vya Sentensi**

Data za utafiti zilizochambuliwa pia zimebainisha kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda, hufanya dosari kwa kutozingatia mpangilio mwafaka wa viambajengo vya tungo kama vile sentensi na virai katika sarufi ya Kiswahili. Kwa mfano, masimulizi ya wajifunzaji yaliyorekodiwa na mtafiti alipokuwa akishuhudia vipindi vya Kiswahili darasani, yamedhihirisha mpangilio usio sahihi wa viambajengo katika tungo kama vile kirai na sentensi kwa

kukifanya kivumishi kitangulie nomino katika kirai nomino badala ya nomino kutangulia kivumishi. Mfano wa data yenye tungo za aina hii ni kama ufuatao:

**Simulizi Na. 5**

> …*ile siku Akida anaenda kuzawadiwa alivaa viato ya Tim. *Hiyo viato ilikuwa plastic, na *hiyo siku ilikuwaka mchana mwingi na alilala barabara. Wizi waliiba *hiyo viato lakini Tim hajali *hayo mambo…

**Chanzo:** Data kutoka Uwandani (2023)

Kutokana na data hii, mjifunzaji alifanya dosari kwa kutumia mpangilio usio sahihi wa viambajengo katika tungo kwa kukifanya kivumishi kitangulie nomino katika tungo. Mifano ya dosari hizo imebainishwa katika jedwali lifatalo:

**Jedwala Na. 9: Mpangilio Usio Sahihi wa Viambajengo vya Sentensi**

| Na. | Tungo zenye Dosari | Tungo katika Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|
| a) | **Ile siku* | Siku ile |
| b) | **Hiyo viato* | Viatu hivyo |
| c) | **Hiyo siku* | Siku hiyo |
| d) | **Hayo mambo* | Mambo hayo |

**Chanzo:** Data kutoka Uwandani (2023)

Tungo zilizobainishwa katika Jedwali Na. 9 hapo juu ni dosari zilizofanywa na mjifunzaji kwa kutumia mpangilio wa viambajengo usio sahihi. Katika tungo hizo, mjifunzaji anafanya dosari kwa kutanguliza kivumishi kioneshi katika kirai nomino badala ya nomino kutangulia kivumishi.

### 4.8 Dosari Kutokana na Utohozi Usiofaa wa Maneno

Halikadhalika, matokeo ya utafiti huu pia yalibainisha kuwapo kwa dosari ambazo hutokana na wajifunzaji kutumia utohozi usiofaa wa maneno. Kulingana na Massamba (2004), utohozi ni uundaji wa istilahi kwa kubadili maumbo ya maneno ya lugha moja na kuyafanya yatamkike kama ya lugha nyingine husika. Kutokana na data za utafuti huu zilizokusanywa kutokana na uandishi wa insha na ushuhudiaji; wajifunzaji walitohoa baadhi ya maneno hasa vitenzi na nomino badala ya kutumia visawe vya maneno hayo katika Kiswahili. Mifano ya dosari za aina hii imeoneshwa katika Jedwali Na. 10 kama ifuatavyo:

**Jedwali Na. 10: Dosari Kutokana na Utohozi Usiofaa**

| Na. | Tungo zenye Dosari | Tungo katika Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|
| a) | **Tamu ilikuwa nzuri* | *Muhula ulikuwa vizuri* |
| b) | **Kilikuwa kiloto changu* | *Ilikuwa ndoto yangu* |

**Chanzo:** Data kutoka Uwandani (2023)

Kutokana na tungo hizi, wajifunzaji walifanya dosari za kimofosintaksia baada ya kutumia utohozi usiofaa. Katika tungo (a) mjifunzaji alitumia neno "*tamu*" ambalo linatoholewa kutokana na *term* katika Kiingereza kurejelea muhula. Katika (b), neno "kiloto" ni nomino na humaanisha "ndoto". Nomino hii imetoholewa kutokana na neno "ekiloto" la lugha zinazozungumzwa nchini Uganda zikiwamo Kiganda, Kinyakitara, Kinyoro-Kitoro na Kifumbira. Utohozi usiofaa wa maneno husababisha dosari za kimofosintaksia pale ambapo hata matumizi yake huathiri viambajengo katika tungo. Kwa mfano, katika tungo (a), matumizi ya neno *"tamu"* yameathiri kiwakilishi "i" na badala ya tungo kuwa *"muhula ulikuwa mzuri"* alisema *"tamu ilikuwa nzuri"*. Aidha, katika (b), matumizi ya nomino "kiloto" yaliathiri kivumishi kimilikishi kilichotumiwa na badala yake tungo kuwa " *kiloto change*" mjifunzaji angesema *" ndoto yangu"*. Hali hii inabainisha kuwa utohozi wa maneno usiofaa huathiri tungo kimofosintaksia.

**4.9 Dosari za Kutokukanusha kwa Usahihi**

Matokeo ya uchambuzi wa data za utafiti huu pia yanadhihirisha kuwa wajifunzaji hufanya dosari zinazotokana na kushindwa kukanusha kwa usahihi. Kutokana na data zilizokusanywa kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji, ilibainika kuwa wajifunzaji huchanganya mofu za ukanushi na wengine hushindwa kuzingatia vipatanishi vya nomino na mofu tofauti za njeo katika hali ya ukanushi. Mifano ya tungo zenye dosari za aina hii imebainishwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali Na.11: Dosari za Kutokukanusha kwa Usahihi**

| Na. | Tungo zenye Dosari | Tungo katika Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|
| a) | Siku ambayo **utaisahu* | *Siku ambayo sitaisahau* |
| b) | *Mimi *pana jua* | *Sikujua/sijui* |
| c) | *Mimi *panaelewa* | *Nilikuwa sielewi* |
| d) | *Mama alikuwa *bado kwenda* | *Mama alikuwa hajaenda* |
| e) | *Nilisema *sinajua* | *Nilisema sijui* |

**Chanzo:** Data kutoka Uwandani (2023)

Kutokana na data za Jedwali Na. 11, wajifunzaji walishindwa kukanusha vilivyo, kwa mfano, katika (a) tungo hii inatokana na zoezi walilopewa wajifunzaji: *"Tunga insha yenye urefu wa maneno yasiyozidi 300 juu ya siku ambayo hutaisahau daima"*. Baadhi ya wajifunzaji walitunga tungo zenye dosari wakikusudia *" Siku ambayo sitaisahau daima"*. Tungo "*pana jua* na *pana elewa"* katika (b) na (c) hutokana na jinsi wajifunzaji wanavyowasikia wazungumzaji

ambao hujitahidi kuzungumza Kiswahili kutokana na mazingira mbalimbali yasiyo ya kielimu. Kwa mfano, wanajeshi hutumia neno *"pana"* kwa maana ya *"hapana"* katika Kiswahili sanifu wakikusudia kumaanisha kinyume cha kufanyika kwa tendo husika. Kulingana na data hizi, ni dhahiri kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda hufanya dosari za kimofosintaksia kutokana na kushindwa kutumia njeo kwa usahihi.

## 5.0 Hitimisho

Makala haya yalilenga kubainisha na kueleza dosari mbalimbali za kimofosintaksia zinazofanywa na wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda. Data za utafiti zilipatikana kutoka uwandani kwa kutumia uandishi wa insha na ushuhudiaji. Uchambuzi wa data uliongozwa na Nadharia ya Usasanyuzi Dosari iliyoasisiwa na Corder, mwaka 1967. Matokeo ya uchambuzi wa data yamedhihirisha kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda hufanya dosari mbalimbali za kimofosintaksia. Dosari hizo ni pamoja na: matumizi yasiyo sahihi ya vipatanishi vya kisarufi vya nomino, matumizi ya viambishi vya nomino yasiyo sahihi, matumizi yasiyo sahihi ya vielezi vya mahali, virejeshi na vivumishi, kuchanganya njeo, mpangilio usio sahihi wa viambajengo katika tungo, utohozi usiofaa pamoja na ukanushi usio sahihi. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu, wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda hufanya dosari mbalimbali za kimofosintaksia katika ujifunzaji wao. Hivyo, makala haya yanatoa wito kwa walimu kumakinikia sana kipengele hiki katika ufundishaji ili kuwawezesha wajifunzaji kukuza kiwango chao cha umuduji na kujifunza Kiswahili kwa ufasaha.

## Marejeleo

Corder, S.P. (1967) "The Significance of Learners' Errors". *International Review of Applied Linguistics in Language Teaching,* Juz. 5: 161-170.

Gawasike, A. (2016) *Ukakamaaji kwa Wajifunzaji wa Lugha ya Kiswahili katika Jamii ya Wakinga.* Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Hepkwony, L.C. (2011) *Matatizo ya Kisarufi Miongoni mwa Wanafunzi wa Kikipsigis Wanaojifunza Kiswahili Sanifu: Mtazamo wa Lugha Kadirifu*. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.

Kamugisha, A. (2020) *Uchunguzi wa Makosa ya Kimofolojia Yanayofanywa na Wahaya Wanapojifunza Kiswahili.* Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Kisakwah, B.A. (2014) *Uchanganuzi wa Dosari na Muundo wa Sentensi: Ulinganisho wa Sentensi Sahili za Kiswahili Sanifu na za Kisuba*. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.

Kitsao, R.S. (2015) *Uchanganuzi wa Makosa ya Kisarufi katika Insha za Wanafunzi wa Shule za Msingi na namna Yanayochangia Matokeo Mabaya ya Mtihani*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Pwani, Kenya.

Leijten, M. na Van Waes, L. (2013) "Keystroke Logging in Writing Research Using Input Log to Analyse and Visualize Writing Proceses". *Written Communication*, Juz. 30(3): 358-392.

Masereka, L.K. (2021) *Athari za Kimofosintaksia za Kikonzo katika Ujifunzaji wa Kiswahili Ikiwa Lugha ya Pili Nchini Uganda.* Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Mukuthuria, M. (2004) *Kuathiriana kwa Kiswahili na Kimeru: Mifano kutoka kwa Wanafunzi wa Tigana, Kenya.* Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Eagerton, Nakuru.

Mutungu, B.N. (2001) *Dosari za Kileksia katika Insha na Chanzo chake: Uchunguzi wa Shule Tano za Upili Wilayani Kiambu*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.

Nyagah, S.K. (2016) *Uchunguzi wa Makosa ya Kifonolojia na Kimofolojia Yanayojitokeza katika Kazi Andishi za Wanafunzi wa Shule za Upili Tigania Jimbo la Meru*. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.

Obara, J.M. (2014) *Uchunguzi wa Makosa Yanayofanywa na Wanafunzi Wazungumzaji wa Lugha ya Ekegusii.* Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.

Ontiende, M.A. (2013) *Athari za Kimofolojia za Kiolusuba katika Matumizi ya Kiswahili Sanifu kama Lugha ya Pili.* Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.

Ontieri, J.M. (2015) "Athari za Kifonolojia za Lugha ya Kwanza katika Kiswahili: Mfano wa Lugha Teule za Kibantu Nchini Kenya". *Mulika,* Juz. 34: 1-13.

Rapando, M. (2005) *Dosari za Kimofosintaksia katika Kazi za Kiswahili Zilizoandikwa na Wanafunzi wa Shule za Upili Jijini Nairobi.* Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.

Rutagwerela, D. (2022) *Dosari za Kisarufi katika Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Pili miongoni mwa Wanafunzi wa Jamii Lugha ya Wahaya.* Tasnifu ya Uzamivu (Hijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Slabakova, R. (2013). "What is Easy and What is Hard to Acquire in Second Language": *A Generative Perspective*. Katika M. Mangando and Adrian (Wah.), *Contemporary Approaches to Second Language Acquisition*. Amsterdam: John Benjamins. Kur. 5-28.

Vincent, S. (2019) *Dosari za Kimofosintaksia Zifanywazo na Wajifunzaji wa Lugha ya Kiswahili wa Jamii Lugha ya Wairaki.* Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Vincent, S. (2020) "Tathmini ya Dosari Zifanywazo na Jamii ya Wairaki katika Ujifunzaji wa Kiswahili". *Kioo cha Lugha*, Juz. 18: 36-56.

Weigle, S. (1999) "Investigating Rate/Prompt Interactions in Writing Assesssment: Quantitative and Qualitative Approaches". *Assessing Writing,* Juz. 6(2):145-178.